# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS – TAMISEMI

## HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

## SHULE YA SEKONDARI USAGARA

**Barabara ya Jamatini, S.L.P. 330 Tanga, Simu: 0784-413494, ,E-mail:usagarasecondary@gmail.com**
**Website:** www.usagarasec.sc.tz

**SIMU- MKUU WA SHULE: 0784 – 413494**

**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0718 – 012812 AU 0717 - 357820**

**Kumb. Na. USS//6/23/JNG/2023/12/….** **TAREHE :13 / 12 / 2023**

---

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI USAGARA HALMASHAURI YA JIJI LA - 2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha KWANZA katika Shule hii mwaka 2024.

Mwanao anatakiwa aripoti Shule Tarehe **02/01/2024** akiwa amejaza fomu zilizoambatanishwa kwa Usahihi pamoja na maelekezo uliyopewa ya kutekeleza.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**2.1. SARE YA SHULE: ( soma kwa makini ukurasa wa pili ) wenye maelezo ya Sare za Shule )**
**2.2. Picha 3 ( Passport size kwa matumizi ya ofisi )**
**2.3. Nakala 1 ya cheti cha kuzaliwa.**
**2.4. Daftari/Counter Book 10, KALAMU, PENSEL, UFUTIO, RULA NA MKEBE WA HESABU.**
**2.5. nauli ya kwenda na kurudi nyumbani na chakula kwa mwanafunzi wa kutwa ni juu ya mzazi/mlezi.**
**2.6. Mzazi / mlezi unawajibika kumpatia matibabu ipasavyo pindi mwanao anapougua.**
**2.7. Ream ya Karatasi Mbili (2) moja A4 na nyingine Ruled .**
**2.8. Kwa kipindi nchote mwanao anaposoma hapa shuleni utashirikiana kwa ukaribu na walimu ili kufanikisha ndoto za mtoto kitaaluma. Fuatilia mwenendo wake kitabia na kitaaluma.**
**2.9. Mahitaji mengine ya kibinaadamu kama yapo.**

## 3.0. MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU SARE YA SHULE YA SEKONDARI USAGARA

### 3.1.WAVULANA:-

(i) Mashati mawili **(2)** meupe ya mikono mifupi na yasiyobana.
(ii) Suruali mbili **(2)** za rangi ya ugoro (**brown)** zenye marinda zisizobana inchi 16 upana wa chini. Kama Rangi zitachanganya ni vyema kuja shule kupata ufafanuzi.
(iii) Viatu vya ngozi, rangi nyeusi, kisigino kifupi na vya kufunga na kamba (sio buti).
(iv) Soksi nyeupe pair mbili .
(v) Sweta liwe rangi ya ugoro (**brown)** la mikono mirefu, shingo ya "**V"** linapatikana Shuleni akihitaji.
(vi) Mkanda mweusi au ugoro usio na urembo wowote wenye buckle iliyowazi katikati.
(vi) Katika bega la shati la mkono wa kushoto iwekwe Baa I ya rangi ya ugoro ikimaanisha kidato cha I.

Mzazi/Mlezi zingatia maelezo ambayo yametolewa hapo juu.

### 3.2.WASICHANA:-

(i) Mashati mawili **(2)** meupe ya mikono mifupi na yasiyobana wala urembo wowote na yenye vifungo mbele.
(ii) Sketi mbili **(2)** ndefu hadi kufunika goti za rangi ya ugoro (**brown)** zilizochanua zenye rinda box mbele na nyuma madogo madogo pembeni. Kama Rangi /mshono vinachanganya ni vyema kuja shule kupata ufafanuzi zaidi.
(iii) Viatu vya ngozi, rangi nyeusi, kisigino kifupi na vya kufunga na kamba (sio buti).
(iv) Soksi nyeupe pair mbili .
(v) Sweta liwe rangi ya ugoro (**brown)** la mikono mirefu, shingo ya "**V"** linapatikana Shuleni akihitaji.
(vi) Katika bega la shati la mkono wa kushoto iwekwe Baa I ya rangi ya ugoro ikimaanisha kidato cha I.

Mzazi/Mlezi zingatia maelezo ambayo yametolewa hapo juu.

### 3.3.KWA WASICHANA WANAOPENDA KUVAA "HIJABU" – MAELEKEZO YA HIJABU NI KAMA IFUATAVYO:-

(i) Shati nyeupe ya mikono mirefu ( pair mbili ) iliyoshonwa kwa kitambaa cha Tetron/Cotton/halua.
(ii) Sketi mbili **(2)** ndefu hadi kifundo cha mguu za rangi ya ugoro (**brown)** zilizochanua zenye rinda box mbele na nyuma madogo madogo pembeni. Zisizopitisha Mwanga. Kama Rangi /mshono vinachanganya ni vyema kuja shule kupata ufafanuzi zaidi.
(iii) Kitambaa cheupe cha kichwani JUBA cha duara kinachoishia mwisho wa mikono ya Tetron/Cotton/halua.
(iv) Viatu vya ngozi, rangi nyeusi, kisigino kifupi na vya kufunga na kamba (sio buti).
(v) Soksi nyeupe pair mbili .
(vi) Sweta liwe rangi ya ugoro (**brown)** la mikono mirefu, shingo ya "**V"** linapatikana Shuleni akihitaji.
(vii) Katika juba chini upande wa kushoto iwekwe Baa I ya rangi ya ugoro ikimaanisha kidato cha I.

Mzazi/Mlezi zingatia maelezo ambayo yametolewa hapo juu.

**NB.** Kama mpaka shule inafunguliwa SARE itakuwa vado kukamilika mwanao Aje na Sare aliyokuwa anatumia shule yake ya Msingi na siyo nguo za Nyumbani.

### 3.4. SARE ZA MICHEZO.

WAVULANA/WASICHANA- Fulana rangi ya kijani au Bluu Zisizo na Maandishi. Na Bukata au Track suit ya kijani/ Bluu. Raba za michezo ni za Rangi yoyote.

## 4.0. VIFAA VYA USAFI

(i) Wasichana walete Soft Broom moja (1) Na fagio la chelewa la mti 1.
(ii) Wavulana walete Squizer 1 na Hard broom 1.

## 5.0. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 5.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa kulingana na ratiba ya shule uliyopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule na Kuvaa sare ya shule wakati wote.
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote pamoja na Kutunza mali za shule;
viii. Ni marufuku mwanafunzi awapo shuleni kumiliki simu au vifaa vyenye ncha kali au kuwa na dawa bila idhini ya daktari.

### 5.2. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

(i) Wizi au kuruka uzio wa shule na Bweni.
(ii) Kutokuhudhuria darasani bila sababu ya msingi / Utoro unaojirudia rudia au utoro sugu;
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo au kukataa Adhabu kwa makusudi;
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
(vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni size ya brashi na zisiwe za mitindo.
(vii) Kufuga ndevu;
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
(ix) Uvutaji wa sigara;
(x) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba au Kusababisha mimba;
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xiii) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
(xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
(xv) Kudharau Bendera ya Taifa au Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**“ KARIBU SANA USAGARA SEKONDARI ”**

…………………………

**A.R. BIRUMO**

**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

PICHA YA MWANAFUNZI

**USAGARA SHULE YA SEKONDARI,**

**S.L.P. 330,**
**TANGA.**
***Kumb Na. USS/9/4*** **TAREHE:….. / ….. / 20……**

**JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………………………………………………**

**A. FOMU YA MWANAFUNZI KUKUBALI SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**

**Mimi ………………………………………………………………………………..nakubaliana na sheria na taratibu zilizoorodheshwa Katika kipengere namba 3 kinachohusu sharia na kanuni za shule na kuzifuata katika kipindi chote nitakapokuwa nasoma shuleni Usagara. Natambua pia kuwa** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. **25** ya mwaka **1978** na inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

**Sahihi ya Mwanafunzi………………………Tarehe….. / …. / 20……. Sahihi ya dole gumba**

***********************************************************************

**B. HATI YA MZAZI KUKUBALI MASHARTI YA SHULE**

PICHA YA MZAZI/MLEZI

**Mimi ………………………………………………………… S. L. P. ………………………………, KATA YA ……………………………………………..**

**Ni Mzazi/Mlezi wa……………………………………………………… Kazi yangu/shughuli nifanyayo ni…………………………………… nimeyasoma masharti yote ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari Usagara na kuyaelewa vizuri. Pia nitasimamia utekelezaji wa sheria za shule alizopewa mwanangu. Najua pia simu, utoro na uchelewaji shuleni pamoja na maendeleo duni kitaaluma shuleni HAVIKUBALIKI.**

**Sahihi………………………………………Tarehe……/…../ 20….** **Sahihi ya dole gumba**

**Namba ya Simu ya Mzazi/Mlezi…………………………………………….Kata anayoishi mzazi / mlezi ………………………………**

**Maelezo haya yamethibitishwa na :-** **<u>Mihuri husika igongwe</u>**

1. **Mtendaji Kata/Kijiji…………………………………………………………Mhuri wa kata…………………………………………………….**

   **Jina la Mtendaji Kata:…………………………………………………Sahihi……………………………Simu:………………………………….**

2. **Mtendaji wa Kitongoji/ Mtaa…………………………………… Jina:…………………………………………… Simu:………………………**

   **Sahihi………………………………………………** **Mhuri wa Mtaa/Kitongoji…………………………………………………………………**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**PART A**

**To Medical Officer: ………………………………………………………………………………………………………………………………**

**MR/MISS.........................................................................................................(Name in full)**

**Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time schooling course.The examinations should include the following categories (I-II) each category or sub-category of which will render the applicant in-eligible in case of a defect. Pregnarcy (category IV) will also render a girl candidate inligible for the course.**

**I.**
- **(a) Eye-sight**
- **(b) Hearing**
- **(c) Limbs**
- **(d) Speech**
- **(e) Venereal Diseases(s)**
- **(f) Leprosy**
- **(g) Epilepsy**

**II. Neurosis**

**III. Other serious disease**

**Signature…………………………………**

**PART B**

## MEDICAL CERTIFICATE

**(To be completed by Government Medical Officer)**

**I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time school course.**

**I.**
- **(a) Eye-Sigh……………………………………**
- **(b) Hearing……………………………………**
- **(c) Limbs……………………………………..**
- **(d) Speech……………………………………..**
- **(e) Venereal Diseases…………………………..**
- **(f) Leprosy……………………………………..**
- **(g) Epilepsy……………………………………**

**II. Neurosis**

**III. Other serious disease**

**Station…………………………………………………………… Signature………………………………………………………………**

**Designation…………………………………………………**

**Date: ……../ ….. / 20……. Rubber Stamp:……………………………………………………**

## Attach the receipt of charges for examing student!